

## **Mdhihiriko wa Ishara Katika Riwaya za Mohammed Suleiman; Kiu na Nyota ya Rehema**

**Dr. Masoud Nassor Mohammed<sup>(\*)</sup>**

### **• ملخص:**

ركّزت هذه المقالة على تجليات الرمز في الرواية السواحلية. موضحة الرموز التي استخدمها الكاتب محمد سليمان في روايته: "حظ رحمة" و"العطش". حيث بيّنت هاتان الروايتان استخدام الرمزية في سياقات مختلفة. ومع ذلك، فقد لا يتمكن بعض القراء من تحديد هذه الرموز وطريقة استخدامها للإشارة إلى مختلف القضايا الاجتماعية والسياسية والاقتصادية. إن صعوبة فهم هذه الرموز التي استخدمها الكاتب في تصويره للقضايا الاجتماعية المختلفة هو ما دفع مؤلف المقالة للتحقيق في هذه الطريقة، والهدف منها مساعدة قراء الأدب السواهيلي على فهم الرسالة التي تحتويها. وقد استخدم الباحث مفهوم علم السيميائية والسيميولوجيا كنظريات في هذه الدراسة للغة الإشارة. وأخيراً، فقد حددت هذه المقالة المواضع المختلفة التي استخدم فيها المؤلف الرمز بشكل فني للإشارة إلى أشياء أخرى.

**الكلمات المفتاحية:** الرمز، الرمزية، الرواية السواحلية، محمد سليمان.

---

<sup>(\*)</sup> Lecturer in Kiswahili Department, The State University of Zanzibar (SUZA)

• **Ikisiri**

Makala hii imeangazia mdhihiriko wa ishara katika uandishi wa riwaya ya Kiswahili. Makala imechunguza ishara zilizotumiwa na mwandishi Mohamed Suleiman katika riwaya zake mbili; *Nyota ya Rehema* na *Kiu*. Riwaya hizi za pekee za mwandishi Mohamed Suleiman zimedhihirisha matumizi ya lugha ya ishara katika miktadha mbalimbali. Hata hivyo, huenda baadhi ya wasomaji wasiweze kung'amua ishara hizo na namna zilivyotumika kuashiria mambo mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kutokueleweka kwa ishara alizotumia mwandishi huyu, katika kusawiri mambo mbalimbali ya kijamii ndiyo jambo lililomsukuma mwandishi wa makala hii kuichunguza mbinu hii, lengo likiwa ni kuwasaidia wasomaji wa fasihi kuufahamu ujumbe uliomo. Dhana ya semiotiki na semiolojia zimetumiwa kama nadharia katika uchunguzi huu wa lugha ya ishara. Hatimaye makala hii imebainisha maeneo mbalimbali ambayo mwandishi kwa ufundi ametumia ishara kuashiria mambo mengine.

**Maneno Makuu:**

Ishara, uashiriaji, riwaya ya Kiswahili, Mohamed Suleiman.

## **1.0 Utangulizi**

Ligembe (2017) anaeleza kuwa, lugha ni nyenzo muhimu ya fasihi. Kwa kawaida lugha huakisi mila na desturi za jamii fulani. Inawalazimu wasomaji na wahakiki wa kazi za fasihi zikiwemo riwaya kuwa na upeo mkubwa wa uchambuzi wa vipengele vya lugha ya kifasihi vikiwemo ishara na istiari. Mara nyingi masuala ya kitamaduni katika jamii huakisiwa kiishara. Kwa sababu hiyo, Ishara inakuwa ni elementi muhimu inayotumiwa na wanafasihi kuzungumzia mambo mbalimbali yanayoihusu jamii. Hutumia kipengele hiki kuonesha ufundi wa kuitumia lugha na kuwakilisha mambo yaliyomazito. Wakati mwingine hufanya hivyo ili kuzuia uwazi na kujiepusha na vikwazo mbalimbali vinavyoweza kuwakuta iwapo wangeyasema mambo hayo bila kificho. Katika makala hii zimebainishwa na kuelezwa ishara mbalimbali zilivyotumiwa na mwandishi Mohamed Suleiman wa riwaya ya *Kiu na Nyota ya Rehema* kuashiria mambo mengine aliyyoyakusudia kuyafikisha kwa jamii.

## **2.0 Dhana ya Ishara na uashiriaji**

Kwa mujibu wa *Oxford Advanced Learners Dictionary* (1989:1304) uashiriaji ni matumizi ya ishara kuwakilisha jambo hasa katika sanaa na fasihi. Nao *American Heritage Dictionary of English* (1969) wameeleza, uashiriaji ni sanaa ya kuwakilisha kitu kwa kutumia ishara mbalimbali zinazokiwakilisha kitu halisi. Kwa maneno mengine tunaweza kueleza kuwa, ishara ni alama nasibu zilizoandikwa au kuchapishwa, ambazo zinatoa maana mpya. Ishara za kifasihi zinaweza kufasiriwa kwa njia tofauti. Ishara hizo zinaweza zisiwe na maana moja kwa mujibu wa miktadha ya matumzi yake. Zinaweza kutoa maana mbalimbali na zote zikachukuliwa kuwa ni maana sahihi za ishara zilizotumiwa. Inaweza kuwa kitu, tendo au wazo fulani ambalo linatumwiwa na mwandishi kuwakilisha jambo jengine. Ishara huwa na uhusiano na maana maalumu zilizokusudiwa.

*Neno, kirai, kishazi, kitu au tokeo linaweza kutumiwa  
kuashiria jambo fulani jengine tofauti na neno au*

*tokeo lenyewe. kwa mfano damu kwa jamii ya Kikristo huashiria maisha, msamaha, ulinzi nk.* (Abrams: 1993:206)

Abrams (aliyetajwa hapo juu) anasisitiza kuwa, ishara ni kitu, mtu au jambo lolote ambalo linasimama kuwakilisha kitu kingine. Katika fasihi, ishara inaweza kufafanuliwa kwa njia nyingi ili kuleta maana tofauti. Kuashiria wakati mwengine ni muhimu tu ndani ya muktadha na hutafsiriwa kuwakilisha watu, maoni, au jambo fulani. Muktadha unapobadilika na ishara hiyo nayo inaweza kubadilika vilevile.

Akifafanua zaidi ishara na uashiriaji, Wamitila (2003) ameeleza kuwa, istilahi ya ishara hutumiwa kuelezea kitu fulani katika kazi ya kifasihi ambacho huwakilisha kitu kingine. Hali hiyo hutokana na uhusiano uliopo baina ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikra fulani katika akili ya msomaji. Fikra hiyo, inaweza kusadifu mawazo ya mwandishi ama isisadifu. Hata hivyo, huwa pia ni tafsiri sahihi ya kifasihi kutokana na muumano na mtiririko wa lugha yenewe ilivyopangwa.

Wamitila (ameshatajwa), amezigawa ishara katika makundi mawili; ishara bia na ishara isiyo bia. Ishara bia ni ile ambayo huweza kutambuliwa na watu wengine popote pale walipo, kwa mfano milima na mabonde huwa ni ishara ya matatizo makubwa yanayomkabili mtu au jamii, msitu mkubwa na giza huashiria hofu, mto huashiria mpito wa maisha, pete ikaashiria ndoa, mvua neema, jua njaa na simba huwa ni ishara ya ukali na ujasiri.

Kundi la pili la ishara kwa mujibu wa Wamitila, ni ishara isiyo bia au ishara ya kipekee: ishara hii hueleweka kutokana na muktadha tu. Hufasiriwa kutokana na jinsi matini ya kifasihi ilivyofinyangwa na mwandishi wake. Huwa ni neno, maneno au kitu ambacho kwa kawaida kama hakijawekwa katika matini hakiashirii jambo lolote. Huimarishwa uashiriaji wake na msuko wa kilugha ya kifasihi iliyotumika. Kwa mfano unaposoma riwaya ya Kezilahabi *Dunia Uwanja wa Fujo* kuna ndege anaeonekana kuruka kwa shida sana, ndege huyu anaashiria kuvunjika kwa

ndoto za mhusika Tumaini juu ya kujiendeleza kibinafsi na kuitafuta furaha ya maisha yake.

Naye, Madumula (2022) anaeleza usuli wa neno *ishara* kuwa limetoka katika lugha ya Kingereza ‘symbol’ ambalo nalo limetokana na ‘symbollein’ la lugha ya Kiyunani likiwa na maana ya alama, nembo au dalili. Ni kitu hai au kisicho hai ambacho huwakilisha kitu kingine. Akifafanua zaidi mawazo ya Coleridge; mshairi maarufu wa Kingereza wa karne ya kumi na tisa, Madumula anaieleza ishara kuwa ni kama vile wasemavyo Waswahili ‘dalili ya mvua ni mawingu’ yaani Waswahili wanapoona mawingu huwa wanaiona mvua. Hivyo neno, maneno au kitu fulani kusawiriwa kuakisi kitu kingine; hali hiyo huitwa ishara na uashiriaji.

Kwa upande wake Msokile (1993: 82) ameieleza dhana ya ishara kuwa ina maana ya alama au dalili. Mohamed (1995:120) yeeye amebainisha kuwa; ishara ni kitu chenye kuishi au kisichoishi. Ni kiwakilishi cha kitu kinachosimama badala ya kitu kingine kwa mfano; rangi nyeupe katika baadhi ya jamii huwakilisha amani na na nyeusi huwakilisha msiba.

Kuilingano na mawazo ya wataalamu mbalimbali walioelezwa hapo juu, ni wazi kuwa ishara ni kipengele muhimu sana kinachotumiwa na wanafasihi katika kuandika kazi zao. Ni vigumu kuepukwa kipengele hicho katika kila kazi ya fasihi na labda ni muhimu kwa waandishi kukizingatia ili kuifanya fasihi iwe fasihi hasa.

### **3.0 Wanafalsafa Waasisi wa Dhana ya Ishara**

Dhana hii ya ishara na uashiriaji imeasisiwa na kuzungumzwa na wataalamu wakubwa kupitia nadharia zao. Mwanafalsafa Pierce (1839--1914) na mwanaismu Ferdinand de Saussure (1857--1913) ni waasisi wa nadharia hii ya uashiriaji. Wametumia istilahi semiotiki au semiolojia inayomaanisha taaluma au sayansi ya ishara katika lugha na mawasiliano kwa ujumla. Taaluma ya semiolojia ilianza kutumiwa na De Saussure tangu mwaka 1894 ambapo alieeleza semiolojia kuwa ni taaluma ya kisayansi

inayotumiwa kuusoma ulimwengu na maisha ya ishara katika jamii.

Kwa upande mwingine, mwanaumuundo De Saussure, ameeleza namna mshikamano wa viungo mbalimbali vyatugenge kama vile neno, kirai, kishazi na sentensi zinavyosaidia kuipa maana matini. Ameeleza kuwa kila kiungo kimoja kinatekeleza jukumu lake maalumu la kujenga ishara za kisarufi.

Kabla ya ishara za neno na maana. De saussure alikwishazungumzia suala la ishara katika kiwango chake cha msingi yaani fonimu zinazojenga maneno. Anaeleza kuwa fonimu katika maneno zipo kinasibu na hazina maana yoyote zaidi ya kuashiria dhana fulani katika maisha ya ulimwengu tulionao. Hivyo ni wazi kuwa, suala la ishara na uashiriaji limeitanda lugha katika viwango mbalimbali vyatugenge kiisumu kabla hata ya kuitazama lugha ya kifasihi ambayo makala hii inaiangazia. Kwa mujibu wa (Cuddon, 1991 :853) Taaluma ya semiotiki inahusishwa na jamii ya Marekani ya kaskazini na semiolojia inahusishwa zaidi ya jamii ya kijadi ya Ulaya.

Katika taaluma ya uchambuzi wa kazi za fasihi, semiotiki inarejelewa kuwa ni mfumo kamili wa ishara na uashiriaji katika matini na alama tunazohitaji kuzifahamu wakati tunapoyasoma matini hayo. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kuwa ishara ni alama nasibu zilizoandikwa, ambazo zinatoa maana tofauti. Makala hii imechunguza alama mbalimbali zilizotumiwa na Mohammed Suleiman katika riwaya zake mbili **Kiu na Nyota ya Rehema**. Kabla ya kuchambua ishara hizo, kwa ufupi makala inamtazama Mohammed Suleiman mwandishi wa riwaya teule.

#### **4.0 Mohamed Suleiman Mohammed**

Mohamed Suleiman amezaliwa mwaka 1943 kijijini Koani wilaya ya kati Unguja. Baada ya miaka 14 alihamia mjini Unguja. Mohamed, 1981 ameeleza kuwa, kazi za Mohamed Suleiman ni maarufu sana Afrika Mashariki. Anatambulika kuwa ni mtu mwenye ujuzi mkubwa wa sanaa ya uandishi wa kazi za fasihi. Mbatia, 2016 ameeleza kuwa, kama Kezilahabi alivyowakilisha

kilele cha upevu wa riwaya Tanzania bara ndivyo Mohamed Suleiman alivyowakilisha kilele hicho visiwani Zanzibar.

## **5.0 Muhtasari wa Riwaya ya Nyota ya Rehema na Kiu**

*Nyota ya Rehema* ni riwaya iliyochapishwa mwaka 1976. Inamzungumzia Rehema, mhusika mkuu wa riwaya hii. Rehema na nyota yake, anazaliwa katika familia ya kitajiri yenyeye asili ya Kiarabu. Kwa jaala ya Mwenyezi Mungu, Rehema anazaliwa akiwa na rangi tofauti na rangi za wazazi wake, si baba wala mama. Hata hivyo, ilibainika baadae kuwa, Rehema alifanana na bibi yake, na kwamba hakupotea katika asili ya familia yake.

Nayo Riwaya ya *Kiu* imechapishwa mwaka 1972. Imeegemezwa katika dhamira kuu ya tamaa. Tamaa za aina mbalimbali zimewasilishwa pamoja na madhara yake. Riwaya inasimulia kisa cha bwana Mwinyi, Idi na Bahati wakiwa ndio wahusika wakuu wakisababisha visa na vituko mbalimbali vinavyojenga dhamira kuu ya tamaa kwa kushirikiana na wahusika wengine. Mwishoni inamalizia kwa kutoweka Bahati baada ya miadi yake na Idi, mhusika mwenzake walioshirikiana kumdhulumu bwana Mwinyi. Bahati alipodai kwa Idi sehemu ya mali ile iliyodhulumiwa inasadikiwa Idi alimuangamiza Bahati na asijulikane kilichomfika mpaka leo.

## **6.0 Ishara katika Riwaya ya Kiu na Nyota ya Rehema**

Katika sehemu hii ya msingi ya makala hii, maneno, sentensi pamoja na elementi mbalimbali zilizotumiwa na bwana Mohamed Suleiman akiwa kuashiria vitu vyengine kama inavyofafanuliwa hapa chini;

### **6.1 Mbwa wa Sulubu (Simba)**

Mwandishi amemsawiri Sulubu akiwa mpenzi mkubwa wa mbwa. Alikuwa na mbwa aliyemwita simba. Simba huyo alikuwa rafiki yake na mlinzi wake kila mahali na kila wakati. Kibandani pake, kondeni kwake, safarini mwake usiku na mchana alimtegemea. Pia alikuwa ni chanzo chake cha kupata taarifa za matukio yaliyotokea au yanayotarajiwa kutokea. Simba alilishwa

vizuri na kupewa huduma zote. Siku moja simba alipewa kuku aliyeuaawa na mnyama. Mwonja asali haonji mara moja. Simba alinogewa na kuku akawa anakamata mwenyewe kuku wazima na kuwala. Kila uchao kuku walipungua katika banda la Rehema.

Siku hiyo,

*Rehema alipokuwa akiwachungia bandani kuku wake wakati wa magharibi alibaini kuwa kifaranga kimoja ambacho alikinunua kwa ajili ya mbegu, kimepungua katika hesabu. Alimweleza Sulubu ambaye alikuwa uwanjani akitia tupa panga lake la kazi. Papo hapo hasira ilipanda katika uso wa Sulubu, na sura yake ikabadilika. Alinyanyuka kwa ghadhabu akalenga panga lake sawasawa na simba aliyekuwa kalala uwanjani, na kuliangusha kwa nguvu zake zote katikati ya mwili wake. Sauti ya mwisho ya simba ilipaa na kupotea angani na kiwiliwili chake kikafyaratuka pande mbili ardhini. Kitu cha mwisho alichokiona Rehema ulikuwa ulimi wa simba ukilamba mchanga... na yeye akaanguka na kuzirai (Nyota ya Rehema: 118)*

Tukio hili halikutokea kwa bahati mbaya. Mwandishi alikuwa akiashiria jambo jengine ambalo nalo lilidhiiri kabla ya kumalizika kwa hadithi. Karim mume wa Salma binti Fuad. Huyu ni kiongozi wa serikali. Alionja dhuluma, dhuluma ikamnogea, akawa hawadhulumu matajiri tu, bali hata masikini na wanyonge waliofika ofisini kwake kutaka huduma za msingi. Hakuwadhulumu watu mbali tu bali hata mkewe bi Salma. Alimdhulumu Rehema na Sulubu kishamba cha Ramwe. Waliponunua sehemu nyininge huko Pakani, Karim alikuwa tayari nacho kukichukua. Hapo ndipo maji yalipozidi unga.

*Ah! maskini alikuwa keshazoea kula mali ya watu. Maradhi kama hayo hayasikii dawa. Na kwa hivyo, panga la Sulubu lililenga sawasawa na kiwiliwili cha mwivi. Shshap ! vipande viwili.*



*A-a-a-gh-gh! Alisikia Rehema. Hapo alitupa ungo wa mboga na kufukuzia mipakani. Mbio...mbio...mbio! Na tena akasimama ghafla. Akamwita mtume wake, utando mweusi ukamgubika machoni, akaanguka na kuzirai....(Nyota ya Rehema:167)*

Tukio hili lenye matendo yanayonasibiana na lile la kwanza, yaliashiriwa kitambo na tabia za mbwa, kupenda kula kuku bila kupewa, namna alivyopigwa panga na namna Rehema katika matukio yote mawili alivyoyapokea. Rehema sehemu zote mbili alizirai. Mwandishi amefanikiwa vizuri kumtumia mbwa wa Sulubu kama ishara kwa Karim kiongozi mwizi mpenda dhuluma na asiyetaka kubadilika.

## **6.2 Nyumba Kubwa na Ndogo (Unyanyasaji)**

Bwana Fuad alioa mke wa pili, bibi Adila. Alimweka katika nyumba kubwa iliyosimama ubavu kwa ubavu na nyumba ndogo aliyokuwa akiishi Aziza, mke wa kwanza. Jambo hili kwa mujibu wa desturi za Waswahili si la kawaida. Ilivyotarajiwa mke mkubwa acae katika nyumba kubwa na mke mdogo awekwe katika nyumba ndogo. Kufanya kinyume cha desturi ilikuwa ni ishara ya wazi ya unyanyasaji uliofanywa na Fuad dhidi ya mke wake wa kwanza bibi Aziza. Mwandishi anasema:

*Aziza mke wa kwanza, ambaye Fuad aliozwa na marehemu baba yake, alikuwa amejikunja katika unyonge wa kutengwa yeye na mwanawe Rahma katika nyumba ndogo iliyosimama ubavu kwa ubavu na nyumba kubwa aliyokuwa akiishi Fuad na Adila.*  
(Nyota ya Rehema: 2)

M pangilio huu wa makaazi kati ya wake wawili wa bwana Fuad, ni ishara ya kiunyanyasaji kwa mke mkubwa, bibi Aziza. Uteuzi wa makaazi baina ya wake wawili halali haukizingatia taratibu sahihi za kiutamaduni. Aziza hakupewa haki zake kubwa na ndogo. Alitengwa na kudharauliwa. Mumewe hakumjali. Alishirikiana na Adila mke mdogo kumhamisha kabisa baadae hata katika hiyo nyumba ndogo aliyopewa kabla.

### 6.3 Kula Sana kwa Sulubu (Nguvu)

Mwandishi anamuonesha Sulubu akiwa anapika na kula kiwango kikubwa cha ugali kinyume na mazoea. Hali hii inaashiria nguvu na uwezo mkubwa wa kufanya kazi. Sulubu alikuwa mchapa kazi hodari. Muda wote alishughulika na kilimo na mifugo bila kuchoka. Alibeba mapakacha makubwa ya mazao kupeleka mjini bila kupumzika popote.

*Rehema alimfuata jikoni, akamwangalia anavyochemsha sufuria ya maji, anavyomimina takriban mfuko mzima wa sembe sufuriani, anavyolisonga, anavyolipakua siniani, anavyochoma pande la nguru mkavu, na anavyolibandika juu ya rumbi la sembe. Lakini walipokuwa wameketi juu ya kuti la kumba huko uwanjani, Rehema hakuweza kula kwani shehena ya boga ilikuwa ingalimo tumboni. Alishikashika tu, akakwanyua ndizi mbivu mbili-tatu katika mkungu wa pukusa uliolazwa kando yao na kumwacha Sulubu akiuvunja ule mlima wa sembe hadi akakutana na sinia lenyewe. (Nyota ya Rehema: 36)*

Ulaji huu haukuwa wa bure uliakisiwa vizuri na utendaji wake wa kazi. Rehema alikuwa anamuona kuwa ni mwanamme madhubuti na alimpenda kwa sababu ya uhodari wake vilevile. Mwandishi alikusudia kuashiria uwezo, nguvu na ujasiri alionao Sulubu katika kazi na utetezi wa haki dhidi ya dhuluma.

### 6.4 Sulubu Ngufumali (Nguvu)

Jambo jingine lililotumiwa na mwandishi ambalo pia ni ishara ya kitu kingine. Ni jina lenyewe alilompa mhusika wake. Mume wa Rehema aliitwa Sulubu Ngufumali/nguvumali. Jina hili ni ishara ya nguvu pia. Mtu mwenye nguvu na anayeweza kustahamili na kuvumilia mikiki yoyote ya kimaisha, kutetea haki zake na haki za wanyonge dhidi ya dhuluma. Sulubu yupo tayari kusulibika ili mradi atimize malengo yake. Nguvumali, ni nguvu zake Sulubu zilizomfanya afaulu katika harakati zake. Nguvu

zilimsaidia katika shughuli za kilimo, katika utetezi wa haki zake na za mkewe. Ni nguvu hizohizo zilizokuwa chanzo cha mapinduzi na kuwapo nafuu wananchi wote kwa ujumla.

### **6.5 Nyamafu (Zinaa)**

Ishara nyingine iliyotumiwa na mwandishi katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* ni neno **nyamafu**. Mwandishi amelitumia neno hili pahala fulani kiishara. Baada ya ruhange kuvamia banda la kuku la Rehema na kuwaua kuku kadhaa. Asubuhi yake Sulubu aliwachukua kuku waliouawa na kwenda nao mtoni kuwatengeneza. Alirudi nao na kuwapika, alionywa na mzee Pongwa asiwale kwani ni haramu kwa utamaduni wa Kiislamu lakini alikaidi na aliwala, akamshawishi na Rehema kula pia. Wote wawili wakafungua vinywa (wakanywa chai) kwa nyamafu. Kwa Rehema habari ya nyamafu haikuishia hapo kwani mwandishi anasimulia hivi:

*Rehema alitambua kuwa amefanya kosa kula nyamafu  
na sasa ilikuwa haitaki kukaa katika tumbo lake.  
Muda mfupi baadae alitapika na kutapika tena. Dawa  
mbalimbali zilitumiwa kujaribu kuzuia asitapike lakini  
hazikufaa chochote. Kumbe haikuwa nyamafu ya kuku  
iliyokuwa ikimtapisha ilikuwa ya Sulubu, Rehema  
alikuwa mjamzito (Nyota ya Rehema: 111)*

Hivyo mwandishi hapo ametumia neno nyamafu kuashiria tendo la zinaa lililofanywa baina ya Sulubu na Rehema kabla ya ndoa. Tendo lililomsababishia ujauzito Rehema na sasa anatapika kwa sababu ya ujauzito huo.

### **6.6 Kutapika (Ujauzito)**

Ishara nyingine iliyotumiwa na Mohamed Suleiman kuashiria jambo jingine ni kutapika. Jambo hili ni la kawaida kwa akina mama wanapokuwa wajawazito. Mara nyingi huwa wanatapika mara kwa mara. Kwa hiyo, hii ni ishara bia kama alivyoitaja Wamiltila. Rehema naye alitapishwa na mwandishi kabla ya kutubainishia ujauzito wake. Muda mfupi baadae taarifa ilipatikana kuwa Rehema ni mjamzito.

*Rehema alitambua kuwa amefanya kosa kula nyamafu na sasa ilikuwa haitaki kukaa katika tumbo lake. Muda mfupi baadaye alitapika na kutapika tena (Nyota ya Rehema: 111)*

Baada ya kuangalia matumizi ya lugha ya ishara pamoja na elementi nyingine zilizotumiwa kiishara katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* ya Mohamed Suleiman hebu sasa na tuangalia dhana hiyo hiyo katika riwaya yake nyengine ya *Kiu*.

## 6.7 Kiu (Tamaa)

Neno **Kiu** ambalo ni jina la riwaya yenyele limetumika kiishara. Ndani ya riwaya hii kuna kiu za aina mbalimbali ambazo zimejengwa juu ya msingi wa tamaa.

*Alikumbuka jinsi miaka mitano hii ilivyoanza na jinsi tamaa ilivyomcheza na jinsi siku zilivyompitia moja baada ya moja zikamwacha katika kiu isiyoburudika. Kiu... ah.. kiu ndiyo kila kitu kiu imeumbwa pamoja na uhai, itaondoka pamoja na uhai.(Kiu: 95 )*

*Kwa hivyo neno kiu katika riwaya ya Kiu limetumiwa kiishara katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:*

Mwandishi amemuonesha bwana Mwinyi akiwa na kiu kubwa ya kimapenzi. Kiu ya kumtia mikononi Bahati awe mpenzi wake. Kiu hii inampa dhiki na hatimaye ugonjwa. Idi dereva wa Mwinyi alipoigundua kiu ya bosi wake, anapatwa naye na kiu yake, kiu ya mali. Anamtumia Bahati kumlaghai Mwinyi ilimradi tu bwana Mwinyi atoe fedha kwa Bahati zitakazowanufaisha katika maisha yao. Bahati naye ingawa hakuwa akipenda alilazimika kukubaliana na Idi kwa kuwa naye alikuwa na kiu ya mapenzi kwa Idi. Bahati alikuwa anampenda kwa dhati Idi. Kwa sababu ya kiu hiyo, alikubali kufanya kila aliloambiwa na Idi ili naye aweze kupendwa.



## **6.8 Zulia Zuri (Utajiri)**

Katika sentensi ya pili tu ya riwaya ya Kiu, mwandishi anataja zulia chini ya nyayo za Mwinyi. Jambo hili linaashiria utajiri mkubwa aliokuwa nao bwana Mwinyi. Utajiri ambao sehemu yake kubwa iliangukia mikononi mwa Idi na mtamanifu mwenzake Bahati. Mwandishi anasema:

*Mwinyi alikuwa ameketi chumbani kwake. Chini ya nyayo zake alikuwa amekanya zulia zuri ambalo thamani yake ingetosha kumfariji maskini kwa siku na miezi.* (Kiu: 1)

Kwa hakika huwezi kukuta zulia kwa mtu maskini na mnyonge ambaye hana uhakika hata wa chakula chake. Hebu tazama mwenyewe Mohamed Suleiman anavyoisifu nyumba ya mtu mnyonge katika riwaya ya Nyota ya Rehema.

*Ingawa paa lake lilikuwa makuti si vigae, kuta zake mbavu za mbwa si saruji, milango yake kumbesa si msaji, matandiko yake dongo na vumbi si mazulia...*  
Rehema angependa kuishi humu kuliko katika kasiri la kwao (Nyota ya Rehema: 23)

Kwa hivyo mwandishi kilitaja zulia katika nyumba ya Mwinyi aliashiria utajiri mkubwa alionao bwana huyo.

## **6.9 Bahati (Matukio)**

Neno bahati katika riwaya hii linaashiria matukio mbalimbali yanayompata binaadamu yawe mazuri au mabaya, ndiyo maana katika Kiswahili kuna bahati nzuri na bahati mbaya. Katika riwaya hii neno hili linamsawiri Bahati ambaye ni mionganoni mwa wahusika wakuu wa riwaya hii. Yeye mwenyewe anakutana na bahati kadhaa ambazo nyingine ni nzuri na nyingine ni mbaya. Hata hivyo, mwisho wake bahati mbaya inatawala maisha yake na unakuwa ndiyo mwisho wa uhai wake. Kama anavyodhihirisha mwandishi;

*Cheusi alianza kutanabahi kuwa mwanawe amekawia kurudi baada ya kupindukia saa tatu za*

*usiku. Aka, ile si desturi yake, alitoka nje na kumwangaza na kumwita na kuwauliza watu hamkunionea bahati huko? (Kiu: 158)*

Cheusi alimtafuta kila mahali bila mafanikio. Siku ya pili kilionekana kikaratasi katika mkoba wake kilichotoka kwa Idi, ambacho kilionesha ahadi ya mukutano wake na bahati lakini Bahati hakuonekana mpaka leo.

Matukio mengine aliyokumbana nayo Bahati ni pamoja na; kukimbiwa na baba yake, kulelewa na mama yake katika maisha magumu, kughilibiwa na Idi kimapenzi kwa tamaa ya fedha, kuolewa na Idi na kunyanyaswa na mumewe kwa kudharauliwa na kuletewa visura (wananwake wa nje) nyumbani kwake.

## **6.10 Kidimbwi cha Maji Ufukweni (ukosefu wa uhuru)**

Mahali pengine katika riwaya ya *Kiu* ambapo mwandishi ametumia ubunifu wa hali ya juu ni kuchora kidimwi cha maji katika ufukwe wa bahari. Kidimbwi hiki kilikuwa na samaki watatu ndani yake, samaki hawa hawakuwa na uhuru wa kutoka ndani ya masafa ya kidimwi hicho. Bahati alikikuta kidimwi hiki, alikichutamia kwa muda. Mwishowe aliamua kuwapa uhuru samaki waliokuwamo mle ndani. Kidimbwi hiki na samaki waliokuwamo ndani kiliashiria ukosefu wa uhuru alionao Bahati. Bahati hakuwa na uhuru wala furaha kutokana na namna alivyofanyiwa na mumewe. Mwandishi anasema:

*... Alikiona kidimbwi alichokuwa akikitafuta, akakiendea na kukichutamia, na akasahau kila kitu. ... Bahati aliwaona samaki watatu wenyewe ukubwa wa kidole chake cha shahada wakihangaika kukimbia kivuli cha yule jinamizi aliyewainamia. ... Bahati aliwatazama na kuwapenda na mara ilimjia hamu ya kutaka kumshika mmoja, amkumbatie kwa vidole vyake ili aweze kuhisi vile anavyoteleza. Alipeleka mkono kidimbwini, lakini wale samaki waliona kivuli kikiwaendea tena na walipaparika kutapia maisha yao*

*hata ilimjia huruma bahati kuwa aliwatendea ukatili.  
Upesi alirudisha mkono wake.*

*...aliwaona mfano wa mahabusu waliofumwa na  
masaibu ya kilimwengu ambayo viumbe wengine pia  
huwafuma au kama yeye yalivyomfuma. Lazima  
awasaidie, ...lazima! Alisimama na kuanza kuupiga  
mateke ukingo wa kile kidimbwi. Akaupiga ,akaupiga,  
akaupiga hata mguu wake ukamwuma halafu bila ya  
kugeuka kuutazama uharibifu wa mateke yake alitoka  
mbio kuelekea mbele zaidi, huku akijirushia tope kwa  
mtimbo wa miguu yake. (Kiu: 101-102)*

### **6.11 Buraha Kando ya Bahari (Ufakhari)**

Baada ya kufanikiwa kumuibia Mwinyi kiwango kikubwa cha fedha, Idi alinunua kiwanja katika mji uitwao Buraha ambao ulikuwa pembezoni mwa bahari. Alidai kuwa anataka kustarehe katika sehemu yenyе utulivu huku akipepewa na upemo wa bahari. Maamuzi haya ya kujenga katika sehemu hii ni ishara ya ufakhari na uwezo waliokwishaupata japo kwa njia haramu. Idi alijiona sasa hastahiki tena kuishi sehemu yoyote tu, lazima akajenge sehemu ambayo wanaishi watu wanaofanana na yeye;

*Nyumba hii? Idi alidharau. Nyumba hii haifai. Tutajenga  
nyengine kando ya mji, sehemu ya pwani.  
Nimekwishapata kiwanja kule buraha. Huoni  
tumekwishapata tabu siku nyingi, na sasa ni wakati wetu  
wa kustarehe? (Kiu: 64)*

Hivyo basi mwandishi aliuchora mji uliokaribu na pwani kuashiria ufakhari na utajiri wa wakaazi wake.

### **6.12 Mzaha (tokeo la kweli)**

Wakati Idi akimtumia Bahati kumuibia Mwinyi pesa zake kwa kumlaghai eti anampenda. Siku moja Bahati alimuandikia Idi barua ya mzaha. Barua ilikuwa hivi:

*Idi usistaajabu nikikwambia ya kuwa hivi sasa niko  
kitandani kwa Bwana Mwinyi, tunapanga siku ya arusi*

*yetu ya kikweli. Si ruhusa kutuingilia kwani tuna hiari yetu. Nakuonya kwa salama yako mwenyewe. Kuwa mipango yako iwe imekoma baada ya kuipata barua hii.*

*Nisalimie fulani...*

*Wa nafsi yangu,*

*Bahati.*

Barua hii ilwasha moto wa hasira kwa Idi, alichanganyikiwa na kuazimia kumuua Bahati. Alipojitokeza Bahati kwani hakuwa mbali naye na kumwambia kuwa alikuwa anamtanía hasira zilishuka. Hata hivyo, alimuonya kutorejea tena utani kama huo. Kwa vyovyyote vile hapa mwandishi alikuwa anaashiria kitu (usaliti). Usaliti wenyewe ulikuja kutokea kweli hapo baadae. Alimdharaau Bahati na hatimaye kumfukuza na kumuangamiza kabisa katika dunia hii.

## 7.0 Hitimisho

Makala hii imezungumzia suala la ishara na uashiriaji katika riwaya mbili za Mohamed Suleiman, makala imedhihirisha ishara mbalimbali zilizotumiwa na mwandishi kuashiria mambo mengine, kuwepo kwa ishara hizo katika riwaya hizi, kumeonesha ufundi wa mwandishi katika kuitumia lugha ya Kiswahili. Aidha imesitisiza kuwa lugha ni mawasiliano ambayo mara nyengine hufumbata mafumbo na ishara za kisitiari zinazobebana.

• **Marejleo**

- Abrams, M.H (1993) *A Glossary of Literary Terms*. London. Holt. RineHart & Winston
- *American Heritage Dictionary of English* (1969) Boston Publishers Houghton Mifflin.
- Cuddon, J.A (1991) *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. London. Penguin Book
- Kezilahabi, E (2007) *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi. Vide/Muwa Publishers Ltd
- Ligembe, N (2017) *The use of Metaphors in Penina Muhando's Lina Ubani: A Stylistic Analysis*. Dar es Salam Afroplus Industries Ltd
- Madumula, J.S (2022) *Riwaya ya Kiswahili*. Toleo la Pili. Dar ES Salaam Afroplus Industries Ltd
- Mohamed Suleiman (1972) *Kiu*. Dar es Salaam. Educational Books Publishers
- Mohamed Suleiman (1976) *Nyota ya Rehema*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- Mohamed, S.A (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi. East Africa Educational Publishers
- Mohamed, S.A (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili*; Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi. Nairobi. East African Educational Publishers Ltd
- Msikile, M (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East African Educational Publishers Ltd
- *Oxford Advanced Learners Dictionary* (1989:1304) Oxford University Press
- Saussure, F (1915) *Course in General Linguistic*. New York. Mac Graw –Hill
- Wamitila, K W (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publishers Ltd.

